

Swahili transcript:

Kwa mfano kama unataka kwenda mikoa mingine, kuna usafiri wa mabasi makubwa. Kwa mfano unataka kwenda mkoa wa Arusha au wa Ruvuma au mkoa wa Dodoma au mikoa mbalimbali, kwa sababu nchi ya Tanzania ina mikoa ishirini na tano, kwa hiyo mikoa ishirini ni Tanzania bara, na mikoa mitano ni Tanzania visiwani ambako tunaita Zanzibar na Pemba. Kwa hiyo kuna usafiri wa mabasi, na kwa upande wa Zanzibar, kwa sababu ni kisiwani kuna usafiri wa meli au ndege. Kwa hiyo tuna usafiri mbalimbali ukitaka kwenda sehemu mbalimbali katika nchi ya Tanzania. Karibuni sana Tanzania kwa sababu usafiri ni mzuri, ukiwa katikati ya miji, au ukitaka kwenda katika mikoa mbalimbali, kuna usafiri mzuri wa mabasi, ukitaka kwenda mikoa ambayo iko aah! ni visiwani, kuna usafiri mzuri wa meli, kuna usafiri mzuri wa ndege, kwa hiyo kuna usafiri pia wa treni. Kwa hiyo kuna usafiri mwingi na ni mzuri na ni raha sana kwa kweli kuishi Tanzania na kutumia usafiri ambao unapatikana Tanzania. Kwa hiyo karibuni sana Tanzania, mje mjionee nchi ya amani na utulivu na kujifunza zaidi watanzania wanavyoishi.

English translation:

If you want to go to other regions in Tanzania, there are bigger buses to travel to the Arusha region, Ruvuma region, Dodoma and other regions. In Tanzania, we have 25 regions. Twenty regions are on mainland Tanzania, and five regions are around the islands of Zanzibar and Pemba. We have bus transportation, but for traveling to the islands, we use boats or planes. As I said, there is no problem with transportation in Tanzania; wherever you want to go, you will go. Welcome to Tanzania. We have different kinds of transportations in the cities, and if you want to go to different regions, we have buses. If you want to go to the islands, you can take a boat or a plane. Also we have trains which help people travel to different regions. So we have many kinds of transportation and it is good to live in Tanzania and use the types of transportation we have. It is so amazing! Once again, welcome to Tanzania. Explore the land of peace and harmony and learn more about how Tanzanians live.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated